# MAHUBIRI KONDOA CATHEDRAL (ACT)

## IBADA YA KUWAPA HESHIMA YA U-CANON.

## 6/8/2023 Saa 3.00 asubuhi

### 1. UTANGULIZI

- Salaam.
- Shukurani kukaribishwa.

Nilipokea mwaliko wa Askofu wa Dayosisi ili kuja kushiriki Ibada hii ya siku ya Bwana, ambayo pia ina tukio la kuwapa heshima ya U-Canon ndugu zetu Wachungaji na Walei pia. Nawapongeza hao wote.

Kitabu cha Sala cha Jimbo letu hakina utaratibu ulio andaliwa kwa Ibada kama hii; lakini kwa kuwa hili ni jambo jema, ninaona ni vizuri kwa Kanisa kuwa na utaratibu wa kuwapokea wahusika kwa heshima hii ya Ucanon, kama alivyofanya Askofu.

Mimi katika kuishi kwangu na kutumika katika Kanisa, nimeona wale walio teuliwa na Askofu hasa wakati wa Sinodi, hata nje ya Sinodi – waliendelea tu kuitwa Ma – Canon, hata bila Ibada maalum.

Aidha, kwa miaka takribani 52 niliyo fanya kazi kama Mchungaji na kisha kama Askofu, sikuwahi kuona ikiitishwa Semina ya Ma-Canon; au hata wakati wa Sinodi, kuelezwa wajibu wa Ma- Canon.
Nakumbuka mara moja tu nikiwa Askofu msaidizi, chini ya Askofu Madinda – DCT, nilipo wahi kuitisha Ma-Canon wote kwa kibali cha Askofu wa Dayosisi. Lakini Askofu wa Dayosisi alikuwa na shaka: Akaniuliza “unataka kuwaambia nini?

Lilikuwa ni swali gumu kwangu kwa sababu sikuwa Canon! Nilitazamia yeye ndiye awaeleze maana na wajibu wa Canon.
Aliniruhusu kuwaita, na yeye akakubali kuwapo.

Mimi nilijiuma uma tu katika maelezo yangu; na yeye akakubali kueleza machache kuhusu Ma-Canon, kisha kutokana na moyo wake wa kupenda Uinjilisti, akatumia muda mrefu kusema juu ya Uinjilisti,

ili Ma-Canon wajue mzigo wake kuhusu kazi ya Uinjilisti katika Dayosisi.
Kwa ushuhuda huo, nipende kusema naona ni jambo jema sana kwa Askofu kuwa na Ibada yenye tukio hili la kutoa heshima ya U-Canon. Ibada hii inatupatia jukwaa la kusema Neno kuhusu nafasi ya Canon katika Kanisa, na kipekee katika Dayosisi.

Najua wapo Wakristo na hata baadhi ya Wachungaji, ambao tungewauliza Canon ni nani, pengine wasingeweza kutoa majibu yanayo tosheleza. Inawezekana hata baadhi ya Ma-Canon wenyewe hawana ufahamu mkubwa, heshima yao inabeba mambo gani. U-Canon siyo cheo, ni heshima katika utumishi katika Kanisa la Kristo.

## 2. SOMO WAEFESO 4:11-16

Mimi nami nilimwomba sana Mungu anipe Neno litakalo endana na siku ya leo.

Nilisukumwa kusoma Neno toka **Waefeso 4:11f**, ambapo inatajwa orodha ya watumishi ambao Bwana Yesu anawatuma duniani kupitia Kanisa lake, kwa ajili ya huduma ya Kanisa.

Huduma hiyo inahusu kuwakamilisha (au kuwawezesha) watakatifu (yaani Wakristo) ili waweze kuitenda huduma ya Bwana vema katika mwili wa Kristo.

Anayetoa vipawa hivyo ni Bwana aliyefufuka.
Wanaopewa ni viongozi katika mwili wa Kristo.
Lengo: **ili luwakamilisha watakatifu (ambao ni mwili wa Kristo**). **Efeso 4:12.**
Vipawa hivyo kwa viongozi, vinatakiwa vitumike kwa ajili ya jamii yote ya Kanisa (Vifungu 12, 13).

Lengo kubwa la hao wanaoitwa na kupewa huo utumishi, ni kuwakamilisha watakatifu, au kwa maneno mepesi, kuwajengea uwezo wakristo, ili nao kila moja wao, kwa kadiri ya karama watakazo pewa na Mungu.

- Waweze kuitenda huduma ya Bwana.

- Waendelee kukua katika imani, wakilenga kujifunza kwake Kristo; ili wasikae katika uchanga, bali wakue hata kufikia kumfahamu sana Bwana Yesu Kristo.

Hili ni jambo kubwa sana kwa yeyote anayeitwa katika utumishi wake Kristo. Lengo lake liwe "hao watakatifu, ambao wana kazi ya kuwa nuru na chumvi duniani".

Hao wajengewe uwezo wa kumjua sana Mungu, ili waweze kutumika kwa huduma watakazo itiwa.

Katika orodha ile wanatajwa:-

- Mitume na Manabii: hawa wanaweka msingi wa Kanisa la Kikristo (**Eph 2:20) "….** Mmejengwa juu ya msingi wa …."
  Wainjilisti: hawa ni wamishenari, wanaopeleka Injili katika maeneo mapya, ambako imani haijahubiriwa.
  Kama **Filipo (Mdo 21:8; 8:6-40**);
  **Timo (2 Tim 4:5)**
  Epaphras pia
- Wachungaji na Waalimu.
  Wachungaji – (hao ni wazee na Maaskofu) -; kulisha, kulinda na kuangalia kundi.
  Waalimu – (hawa pamoja na manabii (**Mdo 13:1)** na **1 Cor 12:28**). Huduma ya kufundisha.
  Kifungu 12f Lengo la huduma zao – kuleta ujumbe wa Neno la Mungu na kufundisha.

Katika **1 Tim 3:1f** wanatajwa Maaskofu na Mashemasi **(Mdo 6:3; Fil 1:1**) Askofu ni mwangalizi na Shemasi ni mtumishi wa Kanisa.

3. **Historia ya "U-Canon" katika Kanisa Anglikana.**

Sasa swali unaloweza kujiuliza je hawa Ma-Canon, wanaangukia kundi gani? Ni nani hawa? Ni wapi katika Biblia wanapotajwa ili na wao wapate faraja kidogo?

Hakuna mahali wanapotajwa Ma-Canon!

**Naomba sasa tulitazame suala la Ma-Canon, kwa kuingalia kwanza historia yake, na jinsi Kanisa Anglikana lilivyoweka huo utaratibu.**

Ni muhimu tufanye hivyo ili tuone kama jambo hilo linabebwa na Neno la Mungu au la!

**Historia na nafasi yao katika Kanisa Anglikana:-**

i. **Neno Canon:**
Ni kama rula (ya kupimia), kigezo, Kanuni (miongozo) zilizowekwa, Desturi, n.k ili watu wafuate.

ii. Hapo awali Neno hilo lilitumiwa kwa Wachungaji wote walio hudumu katika Diocese.
Lakini baadaye likahusu wale wahudumu (Wachungaji) wa Kanisa kuu na wanaolipwa na Kanisa Kuu. Kwa hiyo Mchungaji wa Kanisa kuu akaitwa – Canon wa Cathedral. Neno Canon ni heshima iliyotolewa na Askofu wa Dayosisi kwa Mchungaji (na wakati mwingine kwa Walei).

Lilihusu hasa Wachungaji waliolipwa na Kanisa kuu.

iii. Walikuwepo pia Wachungaji walio itwa Ma-Canon, nje ya wale wa Kanisa kuu. Hawa hawakulipwa mshahara. Lakini waliweza kuwa na nafasi fulani katika Kanisa Kuu, kwa mfano kufanya Ibada; Kazi za Utume na Uinjilisti; na kazi nyingine wakialikwa. Hawa walikuwa na umri mkubwa kazini na wenye uzoefu kati ya Wachungaji.

Walisaidia kazi za Dayosisi kadiri Askofu alivyo elekeza.

**iv.** Mashemasi: Waliweza kupewa heshima ya U-Canon pia.

**Uteuzi / kuchaguliwa**

Canon alichaguliwa au kuteuliwa na Askofu wa Dayosisi.

**Sifa za kuteuliwa**

**Wachungaji:**

- Wanaweza kuteuliwa wale ambao wameisha fikia utumishi usio pungua miaka 6.
- Walio onyesha uaminifu katika utumishi wao kwa miaka kadhaa.
- Maisha yao yana uadilifu, na yenye heshima.

**Mashemasi.**

Mashemasi pia, ambaye amehudumu kwa muda unaozidi miaka 6, aliweza kupewa heshima ya kuwa Canon wa Kanisa kuu. Lakini hawa hawakuruhusiwa kusoma misa au kutoa ghofira.

**Walei.**

Hawa pia waliweza kupewa heshima ya U –Canon, kama walionyesha utumishi wa pekee katika Kanisa. Walipewa heshima hiyo, ili kutambua huduma au utumishi wao wa kipekee.

**Kuna mambo ya kuzingatia hapa kwa wote hao:-**

- Heshima ya U-Canon ilitolewa kwa wale walio tumika na kuishi maisha ya heshima, uaminifu, uadilifu kwa miaka kadhaa, kiasi utumishi wao unavuta heshima.
- Maisha ya mtu anayepewa heshima hiyo yalitakiwa kuwa kielelezo kwa wahudumu wengine kama maana ya neno lilivyo. Walitakiwa kujifunza toka kwa Wachungaji hao (linganisha Maneno ya Mtume Paulo kwa **Timotheo – 2 Tim 2:2; 3:14** na pia **Waebrania 13:7**).
- Kuna wakati heshima hii iliweza kuwa ya muda tu, yaani haikuwa ya maisha yote (kwa mfano mtu akipewa kuwa Canon wa muziki; anapo acha na heshima ya U- Canon anaiacha). Maana alipewa U-Canon kwa kazi maalumu.
- Ma-Canon walikuwa ni wa Kanisa kuu.

**Wajibu wao.**

- **Kusimamia Ibada** za Kanisa kuu.
- **Dean** wa Kanisa Kuu na **Ma-Canon** wote wa Kanisa Kuu **walisimamia utawala wa Kanisa kuu**. **Ndio waliounda "Chapter" au Baraza la Kanisa Kuu.**
- Walikuwa **washauri** wa Askofu Mkuu.
- Walikuwa na wajibu **wa kutunza na kusimamia Kanuni au kawaida zote za Kanisa Kuu**. Kama taratibu za Ibada; mgawanyo wa fedha, majengo, Desturi za Kanisa kuu, Mapambo n.k.
- **Kuhubiri.**

- Kuwa **kielelezo kwa watumishi wengine**.
- **Shughuli** nyingine **watakazo pangiwa na Askofu.**
- Walikuwa na haki ya **kumchagua au kumkataa Askofu aliyeteuliwa**.
- **Mababa wa Kiroho.**

**Angalizo.**
Kama asemavyo Mtume Paulo katika **1 Tim 3:6**, Mhudumu alitakiwa asiteuliwe kabla ya kukua katika imani, bila shaka na katika huduma.

Hii ni tahadhari kwa Askofu mwenyewe. Asiwe na haraka. Awe mwangalifu. Anaweza kupata ushauri wa **Ma-Canon,** kabla ya kutenda.

Asimweke mhudumu kwa sababu tu ni rafiki. Ni hatari maana atakosa ujasiri wa kumshauri.

**4. NAFASI YA CANON LEO.(katika Jimbo letu).**
Sasa baada ya maelezo hayo yote (ya kihistoria), sisi **tunajifunza nini toka katika historia na maelezo hayo?**

**Hapo awali niliuliza swali:** Je ni wapi maandiko Matakatifu yanapo tuelekeza kuhusu kazi ya Canon?

Tukiipekua Biblia hatuwezi kumwona Canon anatajwa, lakini kwa uongozi wa Neno la Mungu, tunaweza kuona kuwa jambo hili halipingani na Biblia.

- Nasukumwa kuona nafasi ya U-Canon ikilinganishwa na ile ya wazee. Viongozi wengi wa Agano la kale walizungukwa na wazee. Kwa mfano Musa – Kutoka **18:12; 24:1** anataja wazee wa Israel, pia wazee 70.

- Katika Agano Jipya;
  Tunaona pia wazee wakitajwa ili kulichunga kundi.
  **Vifungu kama;**
  **Mathayo 15:2** mapokeo ya wazee (walitunza mapokeo)
  **Mdo 20:17 jukumu** la kusimamia na kulisha kundi la Kanisa.
  **1 Pet 5:1f** uchungaji wa kundi.
  **Tito 1:5f** kuonya; kupambana na wazushi
  **1 Tim 5:19** uangalifu katika kushughulikia maadili yao, ni watu wanaobeba heshima.

Sasa ukiangalia

- Namna yao ya kuchaguliwa yaani sifa zao.
- Sababu ya kuwekwa na wajibu wao.

Tunaweza kuona hekima iliyoongoza Kanisa ili wawe na watu ambao watakuwa na nafasi kama ile ya wazee katikati ya jamii ya watoto wa Mungu. Watu wenye sifa za Kiroho, na wenye wajibu unaolenga uchungaji wa kondoo.

- Lakini pia, Biblia inatuambia **Mungu ni wa utaratibu.**
  Kwa mfano tazama:

  **1 Cor 14:33, 40** Mungu si wa machafuko. Mambo yatendeke kwa utaratibu.

  **1 Tim 3:2** Askofu "mzee" awe mtu wa utaratibu.

  **1 Thes 3:6, 7, 11** Paulo anakemea watu wasio na utaratibu.

  **1 Thes 5:14** waonywe wasio kaa kwa utaratibu.

Kwa hiyo ukiangalia Biblia utaona kuwa nafasi hii ya Canon haipingani na Neno la Mungu. Ma-Canon wapo ili kusimamia "utaratibu" katika Kanisa, kama maana ya neno Canon lilivyo.

Tazama hata sifa zao:-

Awe ni mtumishi wa Kanisa.
Mtu aliyejitoa kulitumikia Kanisa.
Mwadilifu.
Maisha yake kuwa kielelezo
Uzoefu kazini (**1 Tim 3:2**) – kuepuka kiburi.

Kwa msingi huo, kwa kuwa hii ni nafasi nzuri, na ya neema na yenye heshima: Ni vema tuwausie MaCanon wetu mambo yafuatayo:-

**a)** Kupewa heshima ya Ucanon, ni jambo kubwa sana. Umeona hata katika historia, walikuwa makini sana nani anapewa heshima hii.

Ni muhimu sana nafasi hii kupewa mtu aliye komaa katika imani; na zaidi mtu aliyekaa katika huduma kwa muda wa kutosha (**1 Tim 3:2**). Hii inampa mamlaka ya kuwa baba wa kiroho kati ya wahudumu wenzake. Anayepewa ajivike **unyenyekevu sana. (1 Pet 5:6).**

**b)** U-Canon ni **heshima** na siyo cheo. Heshima hii haihusu kukaa viti vya mbele, bali kutumika katika Kanisa.

Heshima **inahusu utumishi**, na siyo kufanyiwa kila kitu. Mafundisho ya Bwana Yesu hapa yanaweza kutusaidia, tazama **Luka 22;** na **Yohana 13.** Kuheshimiwa hapa ni sawa na kutambua moyo wa mhusika wa kujituma. Hivyo lazima aendelee kutumika zaidi.

Nafasi yoyote ya Kanisa, iwe ya **uongozi** au **heshima** lazima iwe na **lengo la utumishi "kuwakamilisha watakatifu** (**Waef 4:12**).

**c)** Ma-Canon kama **wazee**, wachukue vielelezo kama vya Barnaba (mtumishi mwenza wa Paulo). Huyu alisimama kama Baba kwa Marko. Alimtia moyo pale alipoona anashindwa kukabili changamoto za utumishi.

Inawezekana Ma-Canon wengine tukaelemea upande wa Paulo, kwa kutompa nafasi Marko (au watumishi wachanga) kukua na kujifunza.

Tukumbuke, huduma yoyote katika Kanisa ipo ili kuwajengea uwezo waumini (watakatifu).

*Hapo zamani baadhi ya Ma-Canon walikuwa tishio sana kwa wahudumu. Walionekana kama watawala. Walisahau wao ni mababa wa kiroho na wachungaji bado.*

**d)** Ma-Canon wanapaswa wazingatie sana wajibu wao wa kuwa **washauri.** Wanapaswa kuutumia vyema huo wajibu, na hasa wanapo mshauri Askofu. Wasilete majungu kwa Askofu, maana watampotosha katika kufanya maamuzi.

Ukiwa msaidizi wa kiongozi na una nafasi ya kumshauri, usitumie vibaya nafasi hiyo. Upo ili kulijenga Kanisa la Kristo, na siyo kulibomoa (tazama tena **Waef 4:12**) au kumpendeza Askofu.

Canon anatakiwa awe mkweli ili kumwezesha Askofu kufanya maamuzi sahihi katika kazi ya Mungu.
(Mfano: **1 Falme 22**: habari za Ahabu na Nabii Mikaya).

**e)** Jambo jingine kubwa ni uhitaji wa Mababa wa kiroho katika Kanisa.

Kanisa linapokosa kuwa na mababa wa kiroho, watu wanaweza kukosa uongozi wa kiroho kati yao. Tazama mfano: **Waamuzi 2:8, 10, 11** pia **2 Timo 1:5;** tazama pia **Waebr 13:7.**

Tunaishi katika nyakati ambapo tukikosa mababa watumishi au wazee (wawe wa kike au kiume) walio na kiroho, Kanisa litapoteza mwelekeo.

Tazama **Efeso 4:14**

Kutulia kwa Kanisa katika siku hizi za mwisho kunategemea sana wale walio na dhamana ya kuchunga, kufundisha na kusimamia kiroho walivyo na uaminifu mbele za Mungu.

Ninyi Ma-Canon ni miongoni mwao.
Simameni katika nafasi yenu. Nirudie kusema heshima yenu ina maana ya kutumika, ili watoto wa Mungu wajengwe katika umoja wa imani kwa ajili ya Bwana.

f. Jambo la mwisho, ni lile analolisema Mtume Paulo katika Waefeso 6:19-20. Wakristo lazima tuwaombee hao M-Canon na watumishi wengine wote wa Kanisa, ili wapewe neema ya kutumika kwa uaminifu katika nafasi wakizoitiwa.

Bwana awabariki.